**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

**SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA**

**S.L.P. 66,**

**NGUDU - KWIMBA**

**Tarehe :...........................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA MKOA WA MWANZA MWAKA ................................**

1. Ninayofuraha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ..................... na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Mwamashimba ipo umbali wa Kilometa 61 Kaskazini/Magharibi/ mwa Mji wa Ngudu. Usafiri wa basi kutoka Jijini Mwanza unapatikana katika kituo cha mabasi Nyegezi kwa nauli ya Shilingi elfu tisa (Tsh.9,000.00). Kama unatokea barabara ya Shinyanga shuka kituo cha mabasi Hungumalwa wilayani kwimba kisha subiri magari yanayotokea Mwanza au Ngudu yanayopatikana kuazia saa sita mchana. Kutoka Hungumalwa ni Kilometa 22 mpaka kibao cha shule, kituo kinaitwa Sanga mbao tatu, nauli ya basi ni shiling elfu nne(Tsh. 4,000.00) na kwa pikipiki ni Shilingi elfu kumi na tatu Tsh. 13,000.00.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ....................... Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............................ Mwisho wa kuripoti ni tarehe ...........................

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1. Sare za Shule**

i. Sketi 2 kitambaa cha suit, rangi ya zambarau (Istim purple) zenye marinda ya kufuatana yenye upana wa inchi 2.5. Sketi ziwe ndefu mpaka kwenye vifundo vya miguu. *kipande cha kitambaa na picha ya mshono vimeambatanishwa na fomu hii.*

ii. Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu, kitambaa cha harua nyeupe.

iii. Hijabu/kijuba rangi nyeupe kitambaa aina ya harua, ifunike kifua cha mwanafunzi. Aidha kwa ndani atavalia shati jeupe aina ya harua la mikono mirefu. *Picha zinazoonesha mshono zimeambatanishwa na fomu hii.*

iv. Soksi jozi mbili nyeupe (stocking).

v. Sare ya Michezo ni Tracksuit rangi ya bluu yenye michirizi mieupe, Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo,T-shirt moja ya bluu aina ya jezi yenye michirizi mieupe mikononi na kola.

vi. Sweta 1 rangi ya bluu isiyo na michirizi lenye nembo la shule.

vii. Tai ndefu zenye rangi ya zambarau zenye michirizi midogo midogo mieupe .

viii. Viatu pair 2 vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi,visivyo na mapambo ya aina yeyote na visivyozidi vifundo vya miguu.

***2.2*** **Sare za Kushindia;** Sketi mbili (2) nyeusi kitambaa cha suit aina ya Istim, zenye marinda ya kufuatana yenye upana wa nchi 2.5 na urefu mpaka kwenye kifundo cha mguu. Juba mbili (2) rangi ya zambarau,Viatu sandles za kimasai na ndala za kuogea**,** T-shirt Mbili (2) za kola, zenye rangi ya kijivu zenye nembo ya shule.

**2.3 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari - Counter book (3quires), yasipungue madaftari nane, 8

ii. Ream mbili (2) za Karatasi **(aina ya double A)** kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);

iv. Scientific Calculator (aina ya casio fx.991); kwa wanaosoma Geography

v. Godoro la wanafunzi kwa vitanda vyetu ni futi 2.5. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari, blanket 1, mto mmoja na foronya zake mbili (2) rangi sawa na mashuka, chandarua 1 mbembe nne(4),rangi nyeupe;

vi. Nguo za ndani za kutosha;

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

viii. Ndoo 2 kubwa na ndogo (moja ya lita ishirini na nyingine lita kumi) kwa matumizi yake, dumu la lita tano(5) kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa na ndoo moja (1) kubwa (lita ishirini) yenye mfuniko kwa ajili ya matumizi ya shule;

**ix.** Vifaa vya usafi; **HKL**;- Kwanja 1, brashi ya chooni na squeezer Cleaning 1; **HGK**;- jembe 1 lenye mpini na reki 1 yenye mpini; **HGL**;- Jembe 1 lenye mpini na mifagio ya ndani (soft & hard bloom). **HGLi**;-Jembe 1 lenye mpini, na grass cutter; **HGFa**;- Mundu, kwanja na brashi ya chooni 1. **Pia Tahasusi zote walete Mifagio ya nje (chelewa ndefu zenye mipini).**

### 2.4 Michango mbalimbali katika shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B:** Lipa fedha zote **Benki ya NMB** au kwa wakala wa **NMB** kwenye akaunti ya shule: jina la akaunti ni **MWAMASHIMBA SECONDARY SCHOOL FUND; akaunti namba 31501100456.**

Aidha mwanafunzi **anatakiwa** kuja na bima ya afya inayotumika ngazi zote za hospitali. Kama hana bima ya aina hiyo, basi aje na **Pesa taslim shilingi elfu hamsini na mia nne(Tshs. 50,400.00)** na uongozi wa shule utamuunganisha na **mfuko wa taifa wa bima ya afya (NHIF)**.

## 3 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya asubuhi na jioni( morning and evening Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule kwa kuzingatia mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**)

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele. Wanafunzi wote katika shule hii wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;

vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

ix. Uvutaji wa sigara;

x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;

xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4 Viambatisho na Fomu Muhimu (ajenavyo Mwanafunzi siku ya kuripoti)**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za passport za mwanafunzi na wazazi/walezi au ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.

v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa

vi. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne 2025(Result Slip)

5 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA**

…………………

**NGOLE M. MWANZALIMA**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

➢ **Mkuu wa shule:0753 557 281 au 0787 557 281**

➢ **Makamu Mkuu wa Shule: 0757 291 207/0623 702 232**

➢ **Mwandamizi Taaluma: 0755 458 998**

➢ **Mwandamizi Malezi: 0766 624 439**

Kiambatisho: A

**KWIMBA DISTRICT COUNCIL**

**MWAMASHIMBA SECONDARY SCHOOL**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

(To be completed by the medical officer in respect of all form five students)

STUDENT'S FULL NAME: ..........................................................................................................

AGE......................................YEARS SEX..............................

STOOL EXAMINATION: ..........................................................................................

BLOOD COUNT (RED AND WHITE): ...........................................................................

URINALYSIS: ..........................................................................................................

SYPHLYSIS TEST: .................................................................................................

T.B TEST: ...............................................................................................................

CHEST: ....................................................................................................................

SPLEEN: ..................................................................................................................

ABNORMAL INFORMATION. eg .physical defects ,impairment ,chronic or family disease etc.

.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
................

I certify that I have examined the above student and recommend that she is fit /unfit to pursue further education.

Signature....................................

Designation................................

Date ............................................ official stamp......................................

(Delete whichever is inapplicable)

Kiambatisho:B

## SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA

## MAELEZO KUHUSU HISTORIA NA MAKAZI YA MWANAFUNZI

### A.MAELEZO BINAFSI

1. Jina la mwanafunzi...............................................Kidato cha .................... jinsia(me/ke)

2. Kabila................................................. Dini..............................................

Tarehe ya kuzaliwa............................ Uraia.............................................

### B.WAZAZI/WALEZI

1. Jina la baba............................................ Je yupo hai ?(NDIYO/HAPANA)

2. Jina la mama......................................... Je yupo hai ?(NDIYO/HAPANA)

3. Kama baba na mama wamefariki /wanaishi mbali:-

a) Jina la mlezi wako..................................kazi ya mlezi…………………………………..

Uhusiano wake na mlezi ni (mjomba, shangazi ,baba mdogo n.k)

b) Kazi ya baba.................................................. Eneo la kazi /idara..................................

c) Kazi ya mama................................................, Eneo la kazi /idara..................................

(d)Je, wazazi wako wanaishi pamoja au wametengana? -.....................................................

### C. MAKAZI YA WAZAZI/WALEZI

a.Baba; mkoa .......................... wilaya ................................., Kata……………, kijiji………………… Mtaa/kitongoji.............................,Namba ya nyumba……. .........................................simu..................................

b.Mama; mkoa .............................., wilaya ..........................., kata……………………., kijiji…………….. kitongoji/mtaa..............................., Namba ya nyumba…………, simu.......................................

c.Mlezi; mkoa .............................., wilaya..............................., kata……………………., Kijiji …...................... kitongoji/mtaa..............................., Namba ya nyumba…………………………………., simu................................

D. Mimi.......................................................... (jina la mwanafunzi )nakiri kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli.

Saini ya mwanafunzi………………………………, tarehe……………………

KIambatisho C:

**FOMU YA KUKIRI KWA MZAZI/MLEZI KUKUBALIANA NA SHERIA, TARATIBU, KANUNI NA MAELEKEZO MBALIMBALI YA SHULE JUU YA MWANAFUNZI.**

Mimi ……………………………………………… ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi

…………………………………………………Nakiri kuwa nimezisoma mbele yake na kuzielewa vyema sheria, taratibu, kanuni na maelekezo mbalimbali atakayopewa mtoto wangu

hapa shuleni.

Nimekubaliana nazo na endapo atafanya kinyume sitamtetea, badala yake nitakubaliana na adhabu atakayopewa kwa kuzingatia sheria hizi.

Na kuheshimu maamuzi yatakayotolewa na uongozi wa shule au walezi wake.

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………

Saini………………………………

Tarehe……………………………

Jina la mwanafunzi………………………………………………….

Saini…………………………………………………………………

Tarehe………………………………………………………………

